

TANGAZO

KATIBU TAWALA MKOA WA SHINYANGA, ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE WENYE SIFA, KUOMBA NAFASI YA KUWA WAJUMBE WA BODI YA USHAURI YA HOSPITALI YA MKOA WA SHINYANGA

WAJUMBE WA BODI HIYO WANATOKA KATIKA MAKUNDI YAFUATAYO:-

1. Mwakilishi kutoka Sekta Binafsi ya Afya
2. Mwanasheria / Wakili
3. Mstaafu katika Fani ya Afya / Ustawi wa Jamii
4. Muwakilishi kutoka katika Taasisi yoyote inayotambulika inayojihusisha na masuala ya Wanawake
5. Muwakilishi kutoka Asasi za Kiraia
6. Mbobezi katika Masuala ya Fedha
7. Muwakilishi wa Huduma za Afya kutoka Ngazi ya Jamii
8. Muwakilishi wa Wananchi kutoka kwenye Jamii
9. Kiongozi wa Dini

SIFA NA KAZI ZA WAJUMBE WA BODI YA USHAURI YA HOSPITALI YA MKOA NI KAMA IFUATAVYO:-

• SIFA ZA JUMLA

1. Mwombaji awe ni mkazi wa Mkoa wa Shinyanga
2. Mwombaji awe tayari kujitolea kufanya kazi za bodi ya ushauri bila kuweka maslahi binafsi
3. Mwombaji awe na elimu kuanzia Shahada ya kwanza au uzoefu katika nafasi anayoiwakilisha
4. Mwombaji awe na uwezo wa kuzungumza na kuandika lugha ya Kiswahili na Kingereza

KAZI ZA KILA MJUMBE

1. Muwakilishi kutoka sekta Binafsi ya Afya

- Kutatua migogoro ya kitabibu
- Kupitisha mikataba inayowekwa na mashirika, Taasisi, sekta Binafsi na watu Binafsi kwa lengo la kuimarisha huduma za Afya
- Kupokea misaada, michango na zawadi kutoka kwa wadau mbalimbali
- Kupitia na kupitisha sera, miongozo na taratibu zinazohusiana na utoaji wa za afya

2. Mwanasheria

- Anawajibika kwa masuala yote ya kisheria yanayohusu Bodi ya Ushauri ya Hospitali ya Mkoa
- Kupitisha mikataba inayowekwa na mashirika, Taasisi, sekta Binafsi na watu Binafsi kwa lengo la kuimarisha huduma za Afya
- Kuiomba Bodi ya Hospitali kuruhusu kufanya uchunguzi maalumu ikiwa ni namna ya kutoa ushauri kwenye changamoto mbalimbali kwa lengo la kuboresha ubora wa huduma za Afya zinazotolewa.

3. Mstaafu katika Fani ya Afya / Ustawi wa Jamii

- Kuwezesha upashanaji wa taarifa kuhusiana na utoaji wa Huduma za Afya, uhamasishaji wa kufuata taratibu na ustawi wa Watumishi.

4. Muwakilishi kutoka katika taasisi yoyote inayotambulika inayojihusisha na masuala ya wanawake

- Kuwezesha upashanaji wa taarifa kuhusiana na utoaji wa Huduma za Afya, uhamasishaji wa kufuata taratibu na ustawi wa Watumishi.
- Kupokea misaada, michango na zawadi kutoka kwa wadau mbalimbali

5. Muwakilishi kutoka asasi za Kiraia

- Kuwezesha upashanaji wa taarifa kuhusiana na utoaji wa Huduma za Afya, uhamasishaji wa kufuata taratibu na ustawi wa Watumishi.

6. Mbobezi katika masuala ya fedha

- Kupitisha bajeti za dharura inapotokea maafa au ajali
- Kupitisha bajeti ya mwaka ya Hospitali
- Kupokea misaada, michango na zawadi kutoka kwa wadau mbalimbali

7. Muwakilishi wa huduma za Afya kutoka ngazi ya jamii

- Kuwezesha upashanaji wa taarifa kuhusiana na utoaji wa Huduma za Afya, uhamasishaji wa kufuata taratibu na ustawi wa Watumishi.

8. Muwakilishi wa wananchi / watumiaji kutoka kwenye jamii

- Kuwezesha upashanaji wa taarifa kuhusiana na utoaji wa Huduma za Afya, uhamasishaji wa kufuata taratibu na ustawi wa Watumishi.

9. Kiongozi wa Dini

- Kuwezesha upashanaji wa taarifa kuhusiana na utoaji wa Huduma za Afya, uhamasishaji wa kufuata taratibu na ustawi wa Watumishi.

MAOMBI YATUMWE KUPITIA ANUANI IFUATAYO;-

KATIBU TAWALA MKOA

S. L. P 320,

SHINYANGA

BARUA PEPE:- ras@shinyanga.go.tz

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 18 Januari, 2019

**Tangazo hili linapatikana pia katika Tovuti ya Mkoa
www.shinyanga.go.tz**